

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA



OFISI YA RAIS
TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA

HALMASHAURI YA WILAYA YA NGARA



Unapojibu tafadhali taja:

Kumb. Na. EB.89/286/02 A/08

26/09/2023

YAH: TANGAZO LA NAFASI ZA KAZI

Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Ngara baada ya kupokea kibali cha Ajira chenye Kumb.Na.FA.170/368/01'C'/96 cha tarehe 22 Agosti, 2023; anawatangazia nafasi ya kazi Watanzania wote wenye sifa za kuajiriwa katika Kada ya **Mtendaji wa Kijiji Daraja la III** kama ifuatavyo:-

1. **Idadi – Nafasi 2.**
2. **Sifa za kuajiriwa - Mwombaji anapaswa kuwa:-**
 - a) Mwenye elimu ya Kidato cha Nne (K.IV) au sita (K.VI).
 - b) Mhitimu wa Mafunzo ya Astashahada/ Cheti katika moja ya fani za Utawala, Sheria, Elimu ya Jamii, Usimamizi wa Fedha, Maendeleo ya Jamii, Mipango na Sayansi ya Sanaa kutoka Chuo cha Serikali za Mitaa Hombolo, Dodoma au Chuo chochote kinacho tambuliwa na Serikali.
3. **Kazi za kufanya – Mwombaji atakayefaulu/ atakayekidhi vigezo na kuajiriwa atafanya kazi zifuatazo:-**
 - a) Afisa Masuuli na Mtendaji Mkuu wa Serikali ya Kijiji.
 - b) Kusimamia Ulinzi na Usalama wa raia na Mali zao; na kuwa Mlinzi wa Amani na Msimamizi wa Utawala Bora katika Kijiji.
 - c) Kuratibu na Kusimamia upangaji wa utekelezaji wa Mipango ya Maendeleo ya Kijiji.
 - d) Katibu wa Mikutano/Vikao na Kamati zote za Halmashauri ya Kijiji.
 - e) Kutafsiri na Kusimamia Sera, Kanuni, Taratibu na Sheria za Nchi.
 - f) Kuandaa Taarifa za Utekelezaji wa kazi katika eneo lake na kuhamasisha Wananchi katika kuandaa na kutekeleza mikakati ya kuondoa njaa, umaskini na kuongeza uzalishaji mali pamoja na kipato binafsi.
 - g) Kiongozi wa Wakuu wa Vitengo vya Kitaalam katika Kijiji.
 - h) Kusimamia, kukusanya na kuhifadhi kumbukumbu zote na Nyaraka za Kijiji.
 - i) Mwenyekiti wa Kikao cha Wataalamu waliopo katika Kijiji.
 - j) Kupokea, kusikiliza na kutatua malalamiko na migogoro ya Wananchi.
 - k) Kusimamia utungaji wa Sheria ndogondogo za Kijiji.
 - l) Atawajibika kwa Mtendaji wa Kata.
 - m) Awe na umri usio zidi miaka 18-45.

4. **Mshahara** – Ngazi ya mshahara na mshahara itakuwa ni:-
TGS/B/.

Mambo muhimu ya jumla ambayo mwombaji anapaswa kuyazingatia ni:-

- (a) Awe Mtanzania Me/Ke mwenye akili timamu
- (b) Barua za mwombaji ziambatishwe pamoja na Vivuli (Photocopies) vya vyeti vya taaluma, ujuzi, kuzaliwa na picha mbili (2) (Passport size) za rangi za hivi karibuni, Nakala ya kitambulisho cha Taifa (NIDA)/ Namba ya NIDA bila kusahau maelezo binafsi (CV) yanayojitosheleza yakionyesha anuani kamili za Wadhamini watatu (3). Namba ya simu ya Mwombaji ni muhimu na iandikwe katika barua ya maombi ya Kazi chini ya anuani yake.
- (c) Waombaji waliosomea nje ya nchi waambatishe uthibitisho wa Vyeti vyao kutoka Baraza la Mitihani la Taifa (NECTA).
- (d) Awe hajawahi kutiwa hatiani kwa makosa ya Jinai.
- (e) Awe hajawahi kupunguzwa/ Kufukuzwa kazi Serikalini.
- (f) Maombi yote yatumwe kwa anuani ifuatayo:-

Mkurugenzi Mtendaji,
Halmashauri ya Wilaya ya Ngara,
S.L.P. 30,
NGARA.

Mwisho wa kupokea maombi ni tarehe **09/10/2023** saa **9:30** alasiri.

Constantino F. Msemwa
KAIMU MKURUGENZI MTENDAJI

- Nakala:**
- i. Katibu Tawala (M),
Ofisi ya Mkuu wa Mkoa,
S.L.P. 299,
BUKOBA – KAGERA.
 - ii. Katibu Tawala (W),
Ofisi ya Mkuu wa Wilaya,
S.L.P. 20,
NGARA.
 - iii. Wakurugenzi wa Mamlaka za Serikali za Mitaa,
MKOA WA KAGERA.
 - iv. Mbao zote za Matangazo,
Halmashauri ya Wilaya,
NGARA.

*MKURUGENZI MTENDAJI
HALMASHAURI YA WILAYA
NGARA*